Notisi ya Desturi za Faragha

**Notisi Hii Itaanza Kutumika Tarehe 1 Oktoba, 2013**

***TAFADHALI IKAGUE KWA MAKINI***

**NOTISI HII INAFAFANUA JINSI TAARIFA YA KUMTAMBULISHA MTU KIBINAFSI INAYOKUHUSU INAWEZA KUTUMIWA NA KUFICHULIWA NA UNAVYOWEZA KUIFIKIA TAARIFA HII.**

Vermont imeanzisha Vermont Health Connect ("VHC") ili kusaidia watu binafsi na mabiashara kununua bima za afya. Moja ya mahitaji ya kuanzisha VHC ni kwamba Vermont inaahidi kulinda usiri wa taarifa ya kibinafsi inayohitaji kusaidia watu binafsi na mabiashara kujisajili kwa bima. Notisi hii ya Desturi za Faragha ("Notisi") inafafanua kile Vermont itafanya ili kulinda taarifa ya kibinafsi.

Notisi hii inatii Sheria ya Ulinzi wa Wagonjwa na Huduma ya Bei Nafuu ("ACA"), inayohusu ukusanyaji, matumizi, ufichuzi na hifadhi ya taarifa inayoweza kumtambulisha mtu ("PII") katika VHC.

Makao ya Vermont Health Connect yatakuwa katika Idara ya Kufikia Huduma ya Kiafya ya Vermont katika Uajenti wa Huduma kwa Watu. Ahadi ya Vermont ya kulinda usiri wa PII unatumika kwa Uajenti wa Huduma kwa Watu na pia kwa makontrakta na wafadhiliwa wake.

**HUDUMA ZA WAKALIMANI BILA MALIPO ZINAPATIKANA**

Tafadhali tuambie ikiwa unahitaji mkalimani au usaidizi mwingine ili uweze kuisoma na kuielewa notisi hii. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

Cette lettre est importante. Si vous ne la comprenez pas, apportez-la a votre bureau local pour recevoir de l'aide. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

Esta carta es importante. Si no la entiende, llevela a su oficina local para solicitor ayuda. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

Ovaj dopis je vazan. Ukoliko je nerazumljiv za vas onda ga ponesite I obratite se lokalnoj kancelariji za pomoc. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

Barua hii ni muhimu. Kama huielewi nenda nayo katika ofisi iliyokaribu kwa msaada zaidi. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

Dokumentigan ama qoraalkan waa muhiim. Haddii aadan fahmin, waxaad u qaadaa xafiiskaaga degaanka si aad caawimaad u hesho. Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

यो दस्तावेज महत्त्वपूर्ण छ। यदि तपाईंले यसलाई बुझ्नुभएन भने, मद्दतको लागि यसलाई आफ्नो स्थानीय कार्यालयमा लिएर जानुहोस्। च्पहं`पउनरू ***1-(855) 899-9600***

ဤစာရွက်စာတန်းသည် အရေးကြီးပါသည်။ သင်နားမလည်လျှင်၊ သင်၏နယ်မြေရုံးခန်းသို့အကူအညီရရန် ယူဆောင်သွားပါ။ Piga simu: ***1-(855) 899-9600***

## DESTURI ZA FARAGHA KUHUSU TAARIFA INAYOWEZA KUMTAMBULISHA MTU

### JE, TAARIFA INAYOWEZA KUMTAMBULISHA MTU ("PII") NI IPI?

Hii ni taarifa yoyote iliyoundwa au kupokewa na Uajenti wa Huduma kwa Watu wa Vermont, makontrakta na wafadhiliwa wake ("AHS") inayoweza kutumiwa kipekee kukutambulisha (kama vile jina lako au nambari yako ya usalama wa kijamii), au inayoweza kutumiwa pamoja na taarifa nyingine inayokuhusu (kama vile jina la ukoo la mama yako) ili kukutambulisha. Mifano ya PII ni:

- Jina
- Nambari ya usalama wa kijamii
- Tarehe na eneo la kuzaliwa
- Anwani
- Nambari ya simu
- Taarifa ya kibaolojia, kama vile alama za vidole
- Anwani ya barua pepe
- Nambari za kadi ya mkopo

**JE, AHS ITAKUSANYA AINA NGANI ZA PII KUTOKA KWANGU KWA AJILI YA VHC?**

Huenda AHS ikakusanya taarifa kama vile jina lako, anwani, nambari ya usalama wa kijamii, taarifa ya ushuru wa shirikisho inayohusu mapato ya nyumba yako, data ya uraia, rekodi za kujisajili, ujauzito, au ulemavu.

AHS **haitakusanya** taarifa ya afya kutoka kwa rekodi zako za kiafya, watoa huduma wako wa afya au watoa bima. Taarifa ya afya iliyoingizwa kwenye VHC, ikiwa kunayo, itakuwa chache na itatoka kwako.

**AHS itafanya nini na PII yangu?**

AHS itakusanya, itatumia na itahifadhi taarifa yako ili ikusaidie kutafuta na kujisajili kwa bima ya afya iliyo ya bei nafuu. AHS itakusanya kiasi kichache cha PII kinachohitajika kutimiza jambo hili.

AHS inaweza kutumia PII yako ili:

- Kuamua ustahiki wa kujisajili katika moja ya mipango ya afya inayofaa kuuzwa kwenye VHC;
- Kuamua ustahiki wa mipango mingine ya manufaa ya kiafya, kama vile Medicaid;
- Kuamua ustahiki wa msaada wa kifedha; na
- Kujihusisha katika shughuli za udhibiti na uboreshaji wa ubora.

**JE, NITAKUWA CHANZO CHA KIPEKEE KWA PII YANGU?**

Sio lazima. AHS inaweza kukusanya baadhi ya taarifa kutoka kwa vyanzo vya data vya Jimbo au Shirikisho, kama vile mpango wa Medicaid au IRS. Baadhi ya data kutoka kwa uajenti wa kuripoti mkopo pia inatumika kuthibitisha utambulisho.

**JE, HAKI ZANGU ZINAZOHUSU MATUMIZI YA PII YANGU NI ZIPI?**

- **Haki ya Kufikia PII.** Unaweza kuomba kuona au kupata nakala kwa wakati muafaka ya PII yako katika fomati unayoweza kusoma. Ili kuhakikisha PII yako haitafichuliwa kwa bahati mbaya, AHS itathibitisha utambulisho wako, au utambulisho wa mtu anayeitisha PII yako ili kuhakikisha umemteua kupokea PII yako. Ili uombe nakala yako ya PII, tafadhali wasiliana na Ofisa wetu wa Faragha kupitia taarifa ya mawasiliano iliyo hapa chini.

- **Haki ya Kusahihisha.** Una haki ya kupinga usahihi au ukamilifu wa PII yako kwa wakati unaofaa, na kuomba kwamba taarifa iliyokosewa irekebishwe au kuomba mabishano hayo yanakiliwe ikiwa ombi lako litakataliwa.

- **Haki wa Uamuzi wa Kibinafsi.** Una haki ya kuwa na fursa busara ya kufanya uamuzi unaofaa kuhusu mkusanyiko, matumizi na ufichuzi wa PII yako. Ikiwa una maswali kuhusu PII yako tafadhali wasiliana na Ofisa wetu wa Faragha kupitia taarifa ya mawasiliano iliyo hapa chini.

- **Haki ya kungupuza matumizi ya PII.** Una haki ya kutarajia kwamba PII yako itaundwa, itatumiwa na kufichuliwa na VHC ili kukamilisha madhumuni machache ya kutafuta na kujisajili katika huduma ya afya ya bei nafuu na kwamba haitatumiwa kwa ubaguzi kinyume na sheria.

- **Haki ya Ubora na Ukamilifu wa Data.** Una hako ya kuchukua hatua busara kuhakikisha kwamba PII yako ni kamilifu, sahii na ya kisasa, haijabadilishwa au kuharibiwa kwa namna isiyofaa.

- **Haki ya Taarifa Zaidi.** Ikiwa ungependelea taarifa zaidi kuhusu haki zako za faragha, una wasiwasi kwamba tumekiuka haki zako za faragha, au hukubaliani na uamuzi tuliofanya kuhusu ufikivu wako kwa PII unaweza kuwasiliana na Ofisi yetu ya Faragha.

**HAKI YETU YA KUBADILISHA SHERIA ZA NOTISI HII**

Tunaweza kubadilisha sheria za Notisi hii wakati wowote. Tukibadilisha Notisi hii, tunaweza kufanya sheria za notisi mpya zitumike kwa watu wote au taarifa yako tunayodumisha, ikiwa ni pamoja na taarifa yoyote tuliyounda au kupokea kabla ya kutoa notisi hiyo mpya. Tutachapisha notisi yoyote mpya kwenye tovuti yetu. Pia unaweza kupata notisi yoyote mpya kwa kuwasiliana na ofisi ya Faragha.

**KWA MASWALI YOYOTE KUHUSU NOTISI HII AU KUHUSU HAKI ZAKO ZA PII, IKIWA NI PAMOJA NA HAKI ZOZOTE ZA RUFAA UNAZOWEZA KUWA NAZO TAFADHALI WASILIANA NA:**

Kituo cha Simu cha VHC
Kwa simu, kwa nambari **(855) 899-9600**, au
Kwa barua pepe, katika AHS.PrivacyandSecurity@State.vt.us